MKAKATI WATAIFA WA KUDHIBITI MAAMBUKIZO MAPYA YA VVU

Na
ELIAZARY D.E NYAGWARU
TACAIDS

DIRA YA KIMATAIFA

- **DIRA YA KIMATAIFA- SIFURI TATU 2015**
- Kusiwe na Vifo vitokanavyo na Maambukizo ya UKIMWI (0 deaths related to HIV and AIDS)
- Kusiwe na Maambukizi mapya (0 New infection)
- Kusiwe na Unyanyapaa na ubaguzi (0 stigma and discrimination)

JANGA LA UKIMWI

- UKIMWI ni janga la kibinadamu na la kimaendeleo pia
- Janga linahitaji mkakati na nia ya dhati kulikabili
- Linahitaji afua mahususi kwa ajili ya kinga, matibabu , na kudhibiti athari zitokanazo na UKIMWI
- Afua hizi zielekezwe kuondoa vichocheo vya maambukizi

UKIMWI KATIKA VYUO VIKUU

- Afua za kudhibiti UKIMWI katika vyuo vikuu:
  i. Jinsi chuo kinavyochangia maambukizi ya VVU katika kutekeleza majukumu yake
  ii. Jinsi maambukizi yanavyoiathiri chuo kutekeleza shughuli zake za msingi
  iii. Mikakati mahususi inayowekwa na chuo kupunguza maambukizi na kukabiliana na athari za VVU

UKIMWI KATIKA VYUO VIKUU

- Wingi wa watu katika vyuo wenye malezi tofauti
- Makundi makuu matatu: wanachuo wanaoingia na kutoka vyuoni baada ya kumaliza masomo
- Wahadhili ambao wana madaraka na mamlaka yataaluma
- Watumishi wengineo

UKIMWI KATIKA…

- Ili chuo kikabiliane na maambukizi :
  i. Sekta ifahamu athari za UKIMWI kwa sekta yenyewe
  ii. Iweke mikakati ya mwitikio dhidi ya UKIMWI katika ajenda ya utekelezaji wa majukumu yake
  iii. Itumie nafasi iliyonayo (Comparative advantages) kuweka mikakati na programu za kuudhibiti

UKIMWI KATIKA….

- Afua za kudhibiti VVU katika vyuo, zilenge:
  i. Kudhibiti maambukizi ya VVU mahali pa kazi kwa ajili ya kulinda afya ya wanachuo, wahadhili na wafanyakazi wake

  ii. Kuchangia mwitikio wa taifa dhidi ya UKIMWI kwa kutumia nafasi iliyonayo – tafiti mbalimbali

  iii. Kuweka mazingira wezeshi ili kufanikisha programu na shughuli za kudhibiti UKIMWI

MAMBO MUHIMU KATIKA MWITIKIO

- Utashi wa dhati kwa viongozi wa juu wa sekta (Management Commitment)
- Uchambuzi wa hali halisi ya maambukizi na kuandaa mpango mkakati
- Uwepo wa mfumo wa uratibu: kamati za kudhibiti UKIMWI katika sekta, waelimisha rika n.k

MAMBO…

- Uraghibishi kwa watumishi ili kuwajengea uelewa wa kushiriki katika programu za kudhibiti UKIMWI na kubadili tabia hatarishi
- Kuweka bajeti kwa ajili ya shughuli za Kudhibiti UKIMWI
- Ufuatiliaji na Tathmini ya afua zote ili kupima mafanikio hasa katika mabadiliko ya tabia ya wanachuo, wahadhili na wafanyakazi wa kawaida

MKAKATI WA KINGA

- Mkakati wa kinga dhidi ya Maambukizi: Mkakati huu unalenga kutekeleza Visheni ya kimataifa :
  i. Kupunguza maambukizi mapya hadi 0
  ii. Kupunguza vifo vitokanavyo na VVU hadi 0
  iii. Kuondoa Unyanyapaa na ubaguzi hadi 0

MKAKATI…

- Inakadiliwa kuwa Watanzania karibu 200,000 wanaambukizwa kwa mwaka kutokana na ngono nzembe
- Mkakati unaweka fursa na mwongozo wa kuimarisha juhudi za kupunguza maambukizi
- Unahimiza uratibu na ushirikiano katika kudhibiti visababishi vya janga hili

MKAKATI…

- Kuibua afua mpya zinazolenga makundi maalumu: biashara ya ngono, ngono ya jinsia moja, wafungwa na mahabusu, watumiaji madawa ya kulevya nk.
- Kuongeza juhudi katika tafiti, mfumo wa taarifa
- Kuhimiza ushirikiano na wadau mbalimbali katika mapambano dhidi ya maambukizi

MKAKATI…

- Kuongeza huduma ya matibabu na msaada kwa watu wanaoishi na VVU
- Kuimarisha huduma majumbani kwa kushirikisha jamii
- Kuongeza juhudi ya kupunguza athari zitokanazo na VVU hasa huduma kwa wajane, wagani, yatima N.k.

MKAKATI…

- Kuwa na mpango wa kudhibiti UKIMWI sehemu za kazi ili kupunguza utaraleshi
- Kuongeza raslimali zinazohitajika kutekeleza mkakati huu
- Kuendeleza elimu ya matumizi sahihi ya kondomu za kiume na za kike
- Kupunguza unyanyapaa na ubaguzi katika jamii

CHANGAMOTO

- Ukanushi, kutojali, na ujuaji (much know)
- Ukosefu wa dhati ya kweli (Commitment) kwa baadhi ya viongozi
- Mifumo dhaifu katika kutekeleza afua za kudhibiti UKIMWI,
- Upungufu wa raslimali fedha
- Kutotambua juhudi zinazofanywa na Waratibu hasa Tume
- Kuchanganya UKIMWI na siasa

CHANGAMOTO…

- Unyanyapaa na ubaguzi
- Huduma hafifu za matibabu na afya kwa ujumla
- Ugumu wa kubadili tabia ya ngono hatarishi
- Ukosefu wa ubunifu wa afua mpya za kudhibiti UKIMWI
- Kuwepo mfumo dume unaojenga tofauti za kijinsia

HITIMISHO

- UKIMWI ni tatizo la kijamii na kimaendeleo pia
- Hata hivyo, mtu binafsi ana wajibu wa kutunza na kulinda afya yake mwenyewe
- Ni vyema afua zilenge kubadili tabia
- Ni wajibu wa serikali kuweka mazingira wezeshi ya kukabliana na janga hili kwa kuimarisha mifumo na huduma

TANZANIA BILA UKIMWI INAWEZEKANA

ILA UKIMWI BILA TANZANIA HAIWEZEKANI

ASANTENI SANA